JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA ELIMU SAYANSI TEKNOLOJIA NA UFUNDI

MTAALA

NA

MUHTASARI WA ELIMU YA AWALI

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA ELIMU SAYANSI TEKNOLOJIA NA UFUNDI

MTAALA

NA

MUHTASARI WA ELIMU YA AWALI

2016

© Wizara ya Elimu Sayansi Teknolojia na Ufundi, 2016

Toleo la Kwanza, 2016

ISBN. 978 - 9976 - 61- 431 - 2

Mtaala na muhtasari huu umetayarishwa na:

Taasisi ya Elimu Tanzania

Kitalu Na 686, Barabara ya Ali Hassan Mwinyi

S.L.P 35094

Dar es Salaam.

Simu:+255 22 2773005/+255 22 277 1358

Faksi: +255 22 2774420

Tovuti:www.tie.go.tz

Baruapepe: director.general@tie.go.tz

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kuiga, kunakili, kutafsiri, kupiga chapa au kutoa andiko hili kwa namna yoyote ile bila idhini ya Kamishna wa Elimu, Wizara ya Elimu, Sayansi Teknolojia na Ufundi.

YALIYOMO

UJUMBE KUTOKA TAASISI YA ELIMU TANZANIA..... v
DIBAJI vi
ORODHA YA MAJEDWALI vii
VIFUPISHO viii
SEHEMU YA KWANZA: MAUDHUI YA MTAALA WA ELIMU YA AWALI..... 1
1.0 UTANGULIZI..... 2
1.1 Usuli..... 2
1.2 Muktadha wa Mtaala wa Elimu ya Awali..... 2
1.3 Dhana ya Elimu ya Awali 3
1.4 Walengwa wa Mtaala..... 3
1.5 Malengo ya Elimu ya Awali..... 3
1.6 Umahiri wa Mtoto 4
1.7 Matamko ya Sera Mbalimbali Kuhusu Elimu ya Awali..... 4
2.0 MITAZAMO YA MTAALA..... 4
2.1 Mtaala unaozingatia Umahiri na Elimu Jumuishi 4
2.2 Falsafa ya Elimu..... 4
2.3 Matumizi ya TEHAMA Katika Ufundishaji na Ujifunzaji..... 5
2.4 Lugha ya Kufundishia Elimu ya Awali..... 5
2.5 Misingi ya Utoaji wa Elimu ya Awali..... 5
2.6 Kipindi cha Mpito kwa Mtoto wa Elimu ya Awali..... 6
3.0 MAUDHUI YA MTAALA..... 6
3.1 Maeneo ya Ujifunzaji..... 6
3.2 Masuala Mtambuka..... 7
4.0 UTEKELEZAJI WA MTAALA..... 8
4.1Taratibu za Utoaji wa Elimu ya Awali..... 8
4.2 Rasilimali 8
4.3 Muda wa Utekelezaji wa Mtaala na Idadi ya Vipindi..... 9
4.4 Mazingira ya Shule ya Awali..... 10
4.5 Ufundishaji na Ujifunzaji 10
4.6 Zana za Ufundishaji na Ujifunzaji 10
4.7 Upimaji wa Maendeleo ya Mtoto 10
4.8 Uthibiti wa Ubora..... 14
4.9 Ufuatiliaji na Tathmini..... 14
4.10 Usimamizi wa Mtaala..... 14
4.11 Mafunzo Endelevu ya Mtaala kwa Walimu..... 14
4.12 Ushiriki waWazazi/Jamii..... 15
4.13 Ubia Kati ya Sekta ya Umma na Wadau Wengine..... 15

SEHEMU YA PILI: MUHTASARI WA ELIMU YA AWALI 16
1.0 Utangulizi 17
2.0 Mpangilio wa Muhtasari..... 17
3.0Maudhui ya Muhtasari..... 18

UJUMBE KUTOKA TAASISI YA ELIMU TANZANIA

Elimu ya Awali ni hatua muhimu katika ujifunzaji wa mtoto. Katika hatua hii, mtoto anajengewa misingi ya ujifunzaji endelevu inayomwezesha kukua kiakili, kimwili, kijamii na kimaadili. Ufanisi katika kumjengea mtoto msingi huu unategemea kwa kiasi kikubwa ubora wa mtaala unaotumika.

Ni suala la kujivunia kuwa na mtaala wa Elimu ya Awali unaoakisi jitihada za serikali katika kuleta mapinduzi ya kiuchumi nchini kupitia sekta ya elimu kama inavyobainishwa katika Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025. Ni matumaini yangu kwamba maudhui ya mtaala huu yatawaongoza watumiaji kutumia fursa waliyonayo kumwezesha mtoto kujenga umahiri utakaomsaidia katika kujifunza na kuyamudu maisha yake. Ninatambua kwamba tunaishi katika jamii ambayo mahitaji yake yanabadilika siku hadi siku kutokana na mabadiliko ya kisayansi, kiteknolojia na kiuchumi. Hivyo, mtaala huu utaboreshwa ili kwenda sambamba na mabadiliko hayo.

Mwisho ninapenda kuwashukuru wadau mbalimbali wa Elimu ya Awali kutoka taasisi mbalimbali za Serikali na zisizo za Serikali ambao kwa namna moja au nyingine wamefanikisha uandaaji wa mtaala huu. Taasisi hizo ni pamoja na Chuo Kikuu cha Agha Khan, Dodoma na Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Dar es Salaam, Vyuo vya Ualimu Butimba na Nachingwea, Shule za Awali Chang'ombe na Mlimani, Idara ya Uthibiti Ubora wa Shule Wizara ya Elimu Sayansi Teknolojia na Ufundi (WESTU) na kanda ya Dodoma, Tume ya Kikristo ya Huduma za Jamii na Baraza za Mitihani la Taifa. Aidha, kwa kuwa mabadiliko ya mtaala ni mchakato unaozingatia mahitaji ya jamii, Taasisi ya Elimu Tanzania inakaribisha maoni ya kuboresha mtaala huu kutoka kwa wadau wote wa elimu. Maoni yote yapelekwe kwa Mkurugenzi Mkuu Taasisi ya Elimu Tanzania.



Dkt Elia Y. D Kibga
Kaimu Mkurugenzi Mkuu
Taasisi ya Elimu Tanzania

DIBAJI

Mtaala ni nyenzo muhimu ya ufundishaji na ujifunzaji katika ngazi yoyote ya elimu. Mtaala bora unaakisi ubora wa elimu itakayotolewa.Mtaala wa Elimu ya Awali umeandaliwa ili kumjengea mtoto umahiri utakaomwezesha kumudu ujifunzaji katika elimu ya msingi na ngazi zingine za elimu. Umahiri utakaojengwa kutokana na mtaala huu utamwezesha mtoto kukidhi mahitaji yake ya ukuaji kimwili, kiakili, kihisia na kijamii. Lengo la mtaala huu ni kumsaidia mwalimu na wadau wengine wa Elimu ya Awali kutoa elimu na malezi yenye viwango vya ubora vinavyokubalika kitaifa na kimataifa.

Mtaala wa elimu ya awali umeandaliwa kufuatia mabadiliko ya Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 2014 inayoelekeza kuwa Elimu ya Awali itatolewa kwa muda wa mwaka mmoja kwa watoto wenye umri wa miaka mitatu hadi mitano. Mtaala huu unamlenga mtoto mwenye umri wa miaka mitano. Hata hivyo, watoto wenye umri wa miaka mitatu au minne wanaweza pia kujiunga na Elimu ya Awali ikiwa itathibitishwa kwamba wana utayari. Aidha, mtaala wa Elimu ya Awali umeandaliwa kwa kuzingatia mabadiliko ya kiuchumi, kisayansi na kiteknolojia ili kukidhi mahitaji ya mtoto wa kitanzania.

Mtaala huu umendaliwa na wataalamu wenye uzoefu katika Elimu ya Awali. Ni matarajio yangu kuwa mtaala huu utamjenga mtoto kuwa mbunifu, mwadilifu, mwenye kujitegemea, kujiamini na mwenye mtazamo chanya katika kutawala mazingira yake.

Prof. Eustella P. Bhalalusesa
Kamishna wa Elimu
Wizara ya Elimu Sayansi Teknolojia na Ufundi

ORODHA YA MAJEDWALI

Jedwali Na 1: Masuala mtambuka katika Elimu ya Awali..... 8

Jedwali Na 2: Umahiri na mgawanyo wa muda na vipindi kwa wiki..... 9

Jedwali Na 3: Vigezo vya kupimwa na viwango vya upimaji katika umahiri..... 12

VIFUPISHO

AZISE	Asasi Zisizo za Serikali
KKK	Kusoma, Kuandika na Kuhesabu
OWM-TAMISEMI	Ofisi ya Rais-Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa
TEHAMA	Teknolojia ya Habari na Mawasiliano
TET	Taasisi ya Elimu Tanzania
UKIMWI	Ukosefu wa Kinga Mwilini
VVU	Virusi Vya Ukimwi
WESTU	Wizara ya Elimu Sayansi Teknolojia na Ufundi

SEHEMU YA KWANZA

MAUDHUI YA MTAALA WA ELIMU YA AWALI

1.0 UTANGULIZI

1.1 Usuli

Taasisi ya Elimu Tanzania (TET) imeandaa mtaala wa Elimu ya Awali ili kuimarisha ufundishaji na ujifunzaji unaoendana na mabadiliko ya utoaji wa elimu na mafunzo yaliyojitokeza kwenye Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 2014. Sera hiyo inaelekeza Elimu ya Awali kuwa ni ya lazima na itolewe kwa muda wa mwaka mmoja kwa watoto wenye umri wa miaka mitatu hadi mitano. Hata hivyo, mtaala huu umeandaliwa kwa ajili ya watoto wa miaka mitano. Aidha, iwapo kuna watoto wenye umri wa miaka mitatu na minne na wana utayari wa kujifunza, wataruhusiwa kujiunga na Elimu ya Awali.

Mabadiliko ya mtaala wa elimu ya awali yamelenga kumwezesha mtoto kujenga umahiri uliobainishwa katika maeneo ya ufundishaji na ujifunzaji. Mabadiliko haya pia yamezingatia msisitizo wa serikali katika kuboresha ufundishaji na ujifunzaji wa stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu (KKK). Mtaala huu umetayarishwa ili kumwezesha mtoto kujenga umahiri utakaomwandaa kujiunga na elimumsingi darasa la kwanza.

Uandaaji wa mtaala umezingatia pia matokeo ya tafiti mbalimbali zinazoonesha kwamba mtoto akijengewa umahiri katika Elimu ya Awali hujifunza vyema katika elimu ya msingi na ngazi zingine za elimu zinazofuata. Aidha, mtaala huu umelenga kukidhi mahitaji ya wadau wa elimu kuhusu ubora wa Elimu ya Awali inayotolewa kwa mtoto.

1.2 Muktadha wa Mtaala wa Elimu ya Awali

Elimu ya Awali ni ngazi ya kwanza katika mfumo rasmi wa elimu nchini Tanzania ambayo hutolewa kwa watoto kabla ya kujiunga na elimu ya msingi. Elimu hii hutolewa kwa lengo la kuwawezesha watoto kujenga umahiri utakaowasaidia kumudu maisha yao ya kila siku na kuwaandaa kwa elimu ya msingi.

Mtaala wa Elimu ya Awali umezingatia mahitaji ya kijamii ya mtoto ili kuchochea ukuaji wake katika nyanja zote. Mahitaji hayo ni kama vile matumizi ya lugha ya Kiswahili, afya bora, uhusiano, michezo, maadili, mila na desturi pamoja na masuala mtambuka. Kuhusu mahitaji ya kiuchumi, mtaala umekusudia kumwezesha mtoto kujifunza kwa vitendo zaidi na kwa kutumia rasilimali zilizopo katika mazingira yake ili kupata maarifa, stadi na mielekeo sahihi itakayomwezesha kujenga misingi ya kujitegemea. Mtaala wa Elimu ya Awali umesisitiza masuala ya Michezo na Sanaa ambayo yatamwezesha mtoto kuwa mbunifu, mdadisi na mwenye uwezo wa kutumia mazingira yake katika kupata mahitaji ya msingi na kutatua matatizo yake.

1.3 Dhana ya Elimu ya Awali

Dhana ya Elimu ya Awali imefafanuliwa katika mitazamo tofauti na wataalamu mbalimbali wa elimu hiyo duniani. Hata hivyo, tafsiri za wataalamu hao zimemtazama mtoto katika mitazamo inayofanana kwa kuzingatia umri wa mtoto, utolewaji wa elimu na mazingira ya kufundishia na kujifunzia. Katika nchi nyingi duniani, elimu hii imekuwa ikitolewa kwa watoto katika makundi makuu mawili; vituo vya kulelea watoto wenye umri ulio chini ya miaka mitatu na Elimu ya Awali inayomwandaa mtoto kujiunga na shule ya msingi kwa wale wenye umri kati ya miaka mitatu hadi mitano. Kutokana na nadharia na tafiti mbalimbali za wataalamu, mtoto wa umri kati ya miaka 0-8 anao uwezo wa kujifunza kadiri ya umri wake katika mazingira rafiki na wezeshi. Kulingana na tafiti mbalimbali, kuna faida nyingi zitokanazo na ubora wa Elimu ya Awali. Faida hizo ni pamoja na:

(i) Afya bora ya mwili na akili ambayo hupunguza gharama za huduma za kijamii hapo baadaye;
(ii) Kuongezeka kwa kipato cha mtu binafsi na taifa kwa ujumla;
(iii) Huleta utengamano wa taifa endapo itatolewa kwa usawa; na
(iv) Kuendeleza haki za msingi za mtoto.

1.4 Walengwa wa Mtaala

Walengwa wa mtaala huu ni watoto wenye umri wa miaka 5 na unajumuisha watoto wa aina zote wakiwemo wenye mahitaji maalumu. Watoto wa miaka 3 na 4 wanaweza kujiunga na Elimu ya Awali iwapo walimu watawafanyia upimaji wa awali ili kubaini kama wana utayari wa kujiunga na Elimu ya Awali.

1.5 Malengo ya Elimu ya Awali

Utoaji wa Elimu ya Awali unalenga kumkuza mtoto kiakili, kimwili, kijamii na kihisa. Hivyo basi, malengo ya Elimu ya Awali yatakuwa:

(i) Kukuza uwezo wa mtoto wa kujifunza kwa kutenda;
(ii) Kujenga uwezo wa mtoto kujitambua, kujiamini, kujithamini na kuthamini wengine;
(iii) Kukuza uwezo wa mtoto katika kutunza mazingira;
(iv) Kukuza uwezo wa mtoto kuthamini na kudumisha tamaduni zinazokubalika katika jamii;
(v) Kubaini mtoto mwenye mahitaji maalumu na kutoa afua stahiki;
(vi) Kumjenga mtoto kiroho na kimaadili;
(vii) Kutoa huduma za msingi kwa mtoto;
(viii) Kukuza stadi za awali za ujifunzaji wa mtoto ; na
(ix) Kukuza stadi za ubunifu na kufikiri kimantiki.

1.6 Umahiri wa Mtoto

Mtaala wa Elimu ya Awali unalenga kukuza umahiri ufuatao:

(i) Kuhusiana;
(ii) Kuwasiliana;
(iii) Kutunza afya;
(iv) Kutunza mazingira ;
(v) Kumudu stadi za kisanii; na
(vi) Kutumia dhana za kihisabati.

1.7 Matamko ya Sera Mbalimbali Kuhusu Elimu ya Awali

Mtaala wa Elimu ya Awali umeandaliwa kwa kuzingatia matamko na maazimio mbalimbali ya kitaifa, kikanda na kimataifa yanayohusu utaratibu na mfumo wa utoaji wa elimu kitaifa na kimataifa. Matamko hayo ni pamoja na;

(i) Falsafa ya Elimu ya Kujitegemea ya Mwaka 1967;
(ii) Mkataba wa Kimataifa kuhusu Haki za Watoto wa mwaka 1989;
(iii) Tamko la Kimataifa kuhusu Elimu kwa Wote la mwaka 1990 na 2000;
(iv) Mkataba wa Afrika kuhusu Haki na Ustawi wa Mtoto wa mwaka 1999;
(v) Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 2014; na
(vi) Mwongozo wa Sera ya Shirika la Kazi Duniani ya Mwaka 2014.

2.0 MITAZAMO YA MTAALA

2.1 Mtaala Unaozingatia Umahiri na Elimu Jumuishi

Mtaala wa Elimu ya Awali unasisitiza kumwezesha mtoto kujenga umahiri ambao unajumuisha maarifa, stadi na mielekeo. Umahiri huu unalenga kukidhi mahitaji ya kielimu na ukuaji wa mtoto. Mtoto ni kiini cha ujifunzaji na msisitizo upo katika kumwezesha mtoto kujenga tabia ya kujifunza katika maisha yake yote. Mtaala huu ni jumuishi kwani unagusa mahitaji ya watoto wote wakiwemo wenye mahitaji maalumu kwa kuwawezesha kukua kulingana na mahitaji yao na uwezo wa kutenda.

2.2 Falsafa ya Elimu

Mtaala huu unazingatia Falsafa ya Elimu ya Kujitegemea kama inavyotajwa kwenye Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 2014. Falsafa hii imekuwa ndio msingi wa utoaji elimu Tanzania tangu mwaka 1967. Tafsiri yake katika Elimu ya Awali inaweka msisitizo katika mambo yafuatayo:

(i) Kutoa elimu inayowiana na mahitaji ya jamii au walengwa;
(ii) Kukuza fikra tunduizi na tabia za udadisi;
(iii) Kujifunza kwa kuhusisha nadharia na vitendo;
(iv) Kukuza kujiamini, kufanya uamuzi na kuthamini utu; na
(v) Kushiriki katika shughuli za uzalishaji mali.

2.3 Matumizi ya TEHAMA Katika Ufundishaji na Ujifunzaji

Sera na miongozo ya kitaifa na kimataifa imetilia mkazo matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) katika tendo zima la ufundishaji na ujifunzaji. Sera na miongozo hiyo hujumuisha Sera ya TEHAMA ya elimumsingi ya mwaka 2007, Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 2014 na Mwongozo wa Shirika la Sayansi, Utamaduni na Elimu Duniani-UNESCO wa mwaka 2013 ambavyo vyote vinasisitiza umuhimu wa matumizi ya TEHAMA katika ujifunzaji bora kwa ngazi mbalimbali za elimu ikiwemo Elimu ya Awali. Ili kuwezesha ufundishaji na ujifunzaji bora, TEHAMA itumike katika kufundisha na kujifunza mambo mbalimbali katika Elimu ya Awali.

2.4 Lugha ya Kufundishia Elimu ya Awali

Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 2014 inatamka kuwa lugha ya Kiswahili na Kiingereza zitatumika katika kufundishia Elimu ya Awali. Mtaala huu utatumika katika shule zinazotumia Kiswahili kama lugha ya kufundishia.

2.5 Misingi ya Utoaji wa Elimu ya Awali

Ifuatayo ni misingi ya utoaji wa Elimu ya Awali:

(i) Elimu ya Awali inahitaji mtaala unaosisitiza michezo kama njia ya kufundishia na kujifunzia;

(ii) Kujengewa mazingira rafiki ili kukuza maarifa, stadi, mielekeo na kukabiliana na changamoto mbalimbali. Mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji ya mtoto ni muhimu yaandaliwe na kupangiliwa vema ili kumwezesha mtoto kuwa mdadisi.

(iii) Watoto wana haki ya kucheza, kushirikishwa, kulindwa na kuthaminiwa;

(iv) Elimu ya Awali inahitaji mwalimu anayefahamu kuwa ukuaji wa kimwili, kiakili, kihisia na kijamii wa watoto ni wa kasi kubwa katika miaka ya awali ili kumjenga mtoto kukua katika ujumla wake;

(v) Elimu ya Awali ikuze uzoefu wa awali wa mtoto katika mambo anayoyafahamu na anayoweza kuyatenda;

(vi) Mtoto asitengwe kwa sababu ya kabila lake, utamaduni, dini, lugha, historia ya kifamilia, mahitaji yake maalumu, jinsi au uwezo wake;

(vii) Wazazi na walimu washirikiane ili kumjengea mtoto mazingira mazuri ya ujifunzaji wake;

(viii) Watoto wapewe fursa ya kucheza michezo iliyoandaliwa na wanayoandaa au kuanzisha wenyewe;

(ix) Kutumia vifaa/zana zinazochochea uchangamshi wa awali wa mtoto; na

(x) Walimu watumie elimu na uzoefu wao katika makuzi, maendeleo na ujifunzaji wa watoto ili kuchunguza na kuchukua uamuzi stahiki.

2.6 Kipindi cha Mpito kwa Mtoto wa Elimu ya Awali

Miaka sita ya mwanzo katika maisha ya mtoto ni muhimu katika ukuaji wake. Uzoefu na mazingira ya kwanza ya mtoto ndiyo yanayoweka msingi wa ukuaji wa baadaye na mafanikio katika shule na maisha. Familia na jamii zina mchango mkubwa sana katika kuwasaidia watoto kuwa tayari kwenda shuleni. Shule zinaweza kuboresha utayari wa mtoto kwa kuwa na uhusiano na mlezi wa watoto au shule za awali na kuhakikisha kunakuwa na mwendelezo mzuri kutoka nyumbani kwenda shule ya awali. Watoto wanaingia shule ya awali wakiwa na uzoefu tofauti, stadi, maarifa, lugha, utamaduni na mila na desturi za familia. Shule zinatakiwa kuwa tayari kukidhi mahitaji tofauti ya watoto katika jamii zao na kuhakikisha kila mtoto anafanikiwa.

Kipindi cha mpito kutoka Elimu ya Awali kwenda elimu ya msingi kwa baadhi ya watoto kinakuwa na changamoto kubwa, hivyo wazazi, walimu na wafanyakazi wa shule wanatakiwa kuwasaidia watoto wakati wa mabadiliko haya ili waweze kuyamudu. Watoto wanahitaji msaada ili wajiamini katika kipindi hiki, hivyo wazazi, walimu na wafanyakazi wa shule wanatakiwa kuongea na watoto kuhusu mabadiliko watakayoyaona, kuwasisitiza kuzungumza iwapo wana tatizo na kuwasaidia kuyajua mazingira mapya.

3.0 MAUDHUI YA MTAALA

3.1 Maeneo ya Ujifunzaji

Ili kumwandaa mtoto kwa ajili ya ujifunzaji katika Elimu ya Awali, ni muhimu kumwezesha mtoto kujenga uwezo katika nyanja zote za ukuaji. Mtaala wa Elimu ya Awali umezingatia maeneo yafuatayo:

(i) Maendeleo ya Kihaiba, Kijamii na Kihisia
Eneo hili humsaidia mtoto kujenga umahiri wa kujitambua, kujijali, na kujali wengine, kujithamini na kuthamini wengine na kuwa na tabia njema kwa ujumla. Eneo hili ni muhimu katika kumwezesha mtoto kufanikiwa katika nyanja zote za kimaisha.

(ii) Maendeleo ya Lugha, Mawasiliano, Kusoma na Kuandika
Eneo hili humuwezesha mtoto kujenga umahiri wa kuwasiliana, kuchangamana na wenzake, na kumpa stadi za awali za kusoma na kuandika. Stadi hizo ni pamoja na kuzungumza na kusikiliza; ufahamu kuhusu maandishi, vitabu, herufi, sauti na maneno.

(iii) Maendeleo katika ubunifu, kujieleza na ujumi
Eneo hili humwezesha mtoto kujenga umahiri katika sanaa kama njia ya kupata na kufikisha ujumbe.Watoto wakipewa fursa ya kufikiri na kubuni vitu kwa kutumia zana na vifaa mbalimbali, hujifunza kuelezea hisia zao, mahitaji yao, uwezo wao na maarifa waliyonayo.

(iv) Maendeleo ya kihisabati na kufikiri kimantiki
Eneo hili humwezesha mtoto kujenga umahiri wa kuhusianisha vitu. Kwa kutumia umahiri atakaojenga kupitia eneo hili, mtoto atajifunza vitendo vya kihisabati kwa ujasiri na kwa kujiamini ambapo itamsaidia katika ngazi za elimu zinazofuata.Vilevile, kufikiri kimantiki kutamsaidia mtoto kuwa na uelewa na kufanya uamuzi sahihi na thabiti. Stadi za msingi za kihisabati ni pamoja na maumbo, kulinganisha na kupima vitu, kuchambua na kupanga vitu, mpangilio wa vitu, namba na kuhesabu.

(v) Maendeleo ya kiafya na kimwili
Eneo hili linampa mtoto nafasi ya kuelewa mwili wake na masuala mbalimbali yanayohusu afya. Baadhi ya masuala muhimu katika eneo hili ni kuhusu chakula bora, usafi binafsi na kanuni mbalimbali za afya.

(vi) Maendeleo katika utambuzi wa mwili na mazingira
Eneo hili la ujifunzaji linamwezesha mtoto kujenga umahiri wa kujali na kutunza mwili wake sambamba na mazingira anamoishi. Eneo hili pia litamwezesha mtoto kujenga uwezo wa kutambua maeneo hatarishi na kuchukua tahadhari kwa usalama wake na wa watu wengine.

3.2 Masuala Mtambuka

Mtaala wa Elimu ya Awali umesisitiza masuala mtambuka mbalimbali ambayo ni Usalama barabarani, Elimu ya VVU na UKIMWI, Haki na wajibu wa mtoto, Elimu ya Jinsia, Stadi za Maisha na Elimu ya Mazingira. Masuala mtambuka haya yamechopekwa katika umahiri mkuu na yatafundishwa katika shughuli mbalimbali za ufundishaji na ujifunzaji. Jedwali lifuatalo linaonesha masuala mtambuka na umahiri mkuu unaobeba masuala mtambuka hayo.

Jedwali Na 1: Masuala Mtambuka katika Elimu ya Awali

Suala Mtambuka	Umahiri Mkuu					
	Kuhusiana	**Kuwasiliana**	**Kutunza afya**	**Kutunza mazigira**	**Kumudu stadi za kisanii**	**Kutumia dhana za kihisabati**
Elimu ya Mazingira			√	√	√	
Elimu ya VVU na UKIMWI	√	√	√	√		
Stadi za Maisha	√	√	√	√	√	√
Elimu ya Usalama Barabarani	√	√			√	√
Haki na wajibu wa mtoto	√	√	√	√		
Elimu ya Jinsia	√	√	√	√	√	√

4.0 UTEKELEZAJI WA MTAALA

Utekelezaji wa mtaala wa Elimu ya Awali utazingatia yafuatayo:

4.1 Taratibu za Utoaji wa Elimu ya Awali

Utekelezaji wa mtaala wa Elimu ya Awali utazingatia taratibu, kanuni na miongozo itakayowasaidia wasimamizi na watekelezaji wa mtaala kuutekeleza ipasavyo. Shule za Elimu ya Awali zinatakiwa kusajiliwa kwa kuzingatia mwongozo ulioandaliwa na WESTU. Utoaji wa Elimu ya Awali ufanyike kwa kuzingatia viwango vya ubora vilivyoainishwa katika Mwongozo wa Uendeshaji na Viwango vya Kutolea Huduma za Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Mtoto wa Tanzania.

Ufundishaji na ujifunzaji utatekelezwa kwa kutumia Muhtasari wa Elimu ya Awali ili kumwezesha mtoto kujenga umahiri uliokusudiwa. Mwalimu anapaswa kuwa mnyumbufu katika kuwaongoza watoto kujifunza kwa kutumia mbinu na zana stahiki za kufundishia na kujifunzia kwa kuzingatia umri na uwezo wa mtoto.

4.2 Rasilimali

Katika utekelezaji wa mtaala huu, upatikanaji wa rasilimali watu na vitu ni muhimu katika kufikia ufanisi wa mtaala.

a) Rasilimali Watu

(i) Mtoto

Mtoto ndiye mlengwa mkuu wa mtaala huu, hivyo utekelezaji wa mtaala uzingatie mahitaji, umri na uwezo wa kila mtoto katika ujifunzaji wake.

(ii) Mwalimu

Mwalimu wa Elimu ya Awali aliyepata mafunzo kutoka katika taasisi inayotambuliwa na serikali ndiye mtekelezaji wa mtaala huu.

(iii) Mwalimu Msaidizi

Mwalimu msaidizi atakuwa ni yule aliyepata mafunzo ya kulea, kuwezesha ujifunzaji wa watoto, usimamizi wa darasa na kutoa ushauri kwa wazazi na jamii kuhusu maendeleo ya mtoto.

b) Rasilimali Vitu

Utekelezaji wa mtaala wa Elimu ya Awali unahitaji rasilimali vitu kama vile miundombinu, samani na zana za kufundishia na kujifunzia. Rasilimali hizo zinatakiwa kuwa za kutosha na zinazokidhi viwango vya ubora vilivyobainishwa katika miongozo mbalimbali ya WESTU. Rasilimali hizo ni lazima ziwe zinazingatia watoto wa aina zote wakiwemo wenye mahitaji maalumu. Aidha, ili mtaala uweze kutekelezwa kwa ufanisi rasilimali fedha ni muhimu ili kuwezesha utekelezaji huo.

4.3 Muda waUtekelezaji wa Mtaala na Idadi ya Vipindi

Elimu ya Awali itatolewa kwa muda wa mwaka mmoja kwa watoto wa umri wa miaka mitano (5). Mwaka wa masomo utakuwa na siku 194 sawa na majuma 39 yenye mihula miwili ya kusoma. Kutakuwa na vipindi 5 kwa siku vyenye dakika 20 kila kimoja. Kutakuwa na jumla ya vipindi 25 kwa wiki.

Katika darasa la Elimu ya Awali, watoto watasoma kwa muda wa saa tatu (3) kwa siku. Kutakuwa na jumla ya vipindi vitano (5) vya darasani ambavyo vitachukua saa moja na dakika arobaini (1:40). Kutakuwa na kipindi kimoja cha dakika 20 ambacho kitatumika kwa shughuli za nje ya darasa kama vile michezo. Vilevile kutakuwa na muda wa mapumziko wa saa moja ambapo watoto watapata muda wa kupata chakula na kucheza. Muda wa kuanza na kumaliza vipindi utategemea mazingira na hali halisi ya sehemu husika.

Jedwali Na 2: Umahiri na Mgawanyo wa Muda na Vipindi kwa Wiki

Umahiri Mkuu	Idadi ya Vipindi kwa Wiki	Muda wa Kujifunza kwa Wiki (Dakika)
Kuhusiana	2	40
Kuwasiliana	6	120
Kutunza afya	6	120
Kutunza mazingira	2	40
Kumudu stadi za kisanii	5	100
Kutumia dhana za kihisabati	4	89

4.4 Mazingira ya Shule ya Awali

Mazingira ya shule ya awali yanaandaliwa kwa namna ambayo watoto watajifunza hata bila mwalimu kuwepo. Katika Elimu ya Awali, mazingira yanayomzunguka mtoto ni mwalimu wa tatu baada ya wazazi na mwalimu wa darasani. Ni muhimu kuandaa mazingira ya ndani na nje kwa kuzingatia falsafa na nadharia za Elimu ya Awali. Mazingira ya ndani na ya nje yatumiwe kwa kusudi la kumpa mtoto nafasi ya kujifunza kwa kutenda.

4.5 Ufundishaji na Ujifunzaji

Mbinu za ufundishaji ni chanzo cha mtoto kupenda kujifunza. Katika shule ya awali ujifunzaji na ufundishaji hufanyika kwa vitendo. Mwalimu anatakiwa kutumia mbinu ambazo zinawashirikisha watoto katika tendo zima la ujifunzaji. Katika Elimu ya Awali, watoto wanajifunza zaidi kupitia michezo kwa kuwa michezo ndiyo shughuli kuu ya watoto. Faida za michezo ni pamoja na:

(i) Kumkuza mtoto katika nyanja zote za ukuaji (kiakili, kimwili, kijamii na kihisia);
(ii) Kujenga misuli mikubwa na midogo ya mtoto;
(iii) Kuleta furaha kwa watoto;
(iv) Kujenga uhusiano baina yao;
(v) Kujenga stadi ya utatuzi wa matatizo;
(vi) Kujifunza kufuata taratibu na kanuni za michezo; na
(viii) Kujenga ubunifu na kukuza udadisi.

4.6 Zana za Ufundishaji na Ujifunzaji

Ufundishaji na ujifunzaji wa mtoto unategemea sana matumizi ya zana stahiki. Shule ya awali inatakiwa kuwa na zana za ndani na nje ya darasa. Zana hizo zinatakiwa ziwe safi, salama na za kuvutia; ziendane na umri, uwezo na mahitaji ya mtoto; ziwe imara na za kudumu, ziwe zinazochochea ugunduzi na udadisi. Mwalimu anatakiwa kuwa mbunifu ili kutumia zana za kufundishia na kujifunzia zinazotokana na mazingira yanayomzunguka.

4.7 Upimaji wa Maendeleo ya Mtoto

Upimaji katika Elimu ya Awali unamwezesha mwalimu kufuatilia maendeleo ya mtoto kuanzia anapoanza darasa la Elimu ya Awali hadi anapohitimu. Upimaji huu utazingatia ukuaji wa mtoto katika nyanja zote za makuzi ya mtoto (kiakili, kimwili, kihisia na kijamii). Lengo la upimaji katika Elimu ya Awali ni kuangalia mchakato wa ujifunzaji wa mtoto na kupima matokeo ya ujifunzaji huo ili kuweza kutoa maamuzi sahihi na msaada unaohitajika. Hivyo, ujifunzaji na upimaji vinakwenda sambamba.

4.7.1 Aina za Upimaji

Upimaji wa maendeleo ya mtoto utafanyika kwa kuzingatia aina kuu tatu za upimaji zifuatazo:

a) Upimaji wa Awali

Upimaji huu hufanywa na mwalimu wa darasa la awali kubaini uzoefu wa awali wa mtoto na vitu anavyoweza kuvifanya. Upimaji huu utafanywa mara tu mtoto anapofika shuleni kwa mara ya kwanza ili kubaini uwezo alionao kabla ya kuanza Elimu ya Awali. Aidha, upimaji utamwezesha kubaini mahitaji binafsi ya mtoto, kutoa afua stahiki pamoja na kuandaa mpango wa kumwezesha kufikia malengo yaliyokusudiwa. Upimaji huu pia unatumika kubaini watoto wenye miaka mitatu na minne ambao wana utayari ili waweze kujiunga na Elimu ya Awali.

b) Upimaji Gunduzi na Chekeche

Upimaji gunduzi ni sehemu ya upimaji endelevu unaolenga kupata taarifa kuhusu uwezo wa mtoto katika kumudu stadi mbalimbali. Taarifa za upimaji huu zitatumika katika kutoa msaada na ushauri stahiki katika malezi, makuzi na maendeleo ya mtoto. Pamoja na upimaji gunduzi, upimaji chekeche utatumika kubaini mtoto mwenye vikwazo vya kujifunza ili kuchukua hatua za kumsaidia.

c) Upimaji Endelezi

Upimaji endelezi unafanyika wakati wote wa ufundishaji na ujifunzaji ndani na nje ya darasa. Upimaji huu utamsaidia mwalimu kubaini ufanisi katika utendaji wa shughuli mbalimbali za kila siku za watoto.

Upimaji wa mtoto hautahusisha mitihani ya kuandika wala hatalinganishwa na mtoto mwingine, bali utazingatia uchunguzi wa mabadiliko yanayojitokeza kwa mtoto kulingana na kile anachotenda kila siku. Mbinu zitakazotumika katika mchakato wa upimaji wa mtoto ni pamoja na uchunguzi, maswali na majibu, picha zinazoonesha matukio mbalimbali ya ujifunzaji wa mtoto, kurekodi sauti na video. Zana za upimaji wa maendeleo ya mtoto ni pamoja na orodha hakiki, mkoba wa kazi, hojaji, jalada na fomu ya maendeleo ya mtoto.

4.7.2 Matokeo ya Ujifunzaji na Viwango vya Upimaji

Mafanikio ya utekelezaji wa mtaala yatapimwa kwa kuangalia kiwango cha ujifunzaji na utendaji wa mtoto. Vigezo vya kupimwa na viashiria vya utendaji vitakavyozingatiwa ni vile vinavyotokana na umahiri mahususi kama vilivyoainishwa katika jedwali hapa chini.

Jedwali Na 3: Vigezo na Viwango vya Upimaji katika Umahiri

Umahiri Mkuu	**Vigezo vya Kupimwa**	**Viashiria vya Upimaji**
Kuhusiana	Uwezo wa kujali	Kujitambulisha Kushirikiana katika kazi mbalimbali
	Uwezo wa kujiheshimu	Kusalimia, Kuonesha tabia njema Kuvaa mavazi yanayokubalika
	Uwezo wa kujitawala	Kujitegemea, Kutawala hisia zake Kutunza vitu vyake
Kuwasiliana	Uwezo wa kusikiliza	Kusikiliza sauti, hadithi, nyimbo Kutoa ujumbe kwa usahihi
	Uwezo wa kuzungumza	Kujieleza Kushiriki katika mazungumzo Kusimulia hadithi
	Kumudu stadi za awali za kusoma	Kusoma picha, Kutamka sauti za irabu na konsonanti Kutambua maumbo ya herufi (irabu na konsonanti)
	Kumudu stadi za awali za kuandika	Kushika viandikio Kuchora mistari Kuumba maumbo ya herufi (irabu na konsonanti)
Kutunza Afya	Kubainisha sehemu za nje za mwili na kazi zake	Kutaja sehemu za mwili Kueleza kazi za sehemu za nje za mwili Kueleza matumizi ya milango ya fahamu
	Kutunza mwili	Kusafisha sehemu za mwili Kuonekana msafi
	Kutunza mavazi	Kufua nguo ndogondogo na nyepesi Kutunza mavazi Kuwa nadhifu
	Kutunza vyombo vya chakula	Kusafisha vyombo Kuhifadhi vyombo
	Kubainisha chakula bora	Kutaja makundi chakula bora
	Kubainisha magonjwa	Kutaja magonjwa, Kutaja vyanzo vya magonjwa hayo Kueleza namna ya kujikinga

Umahiri Mkuu	**Vigezo vya Kupimwa**	**Viashiria vya Upimaji**
Kutunza Mazingira	Kubaini vitu vilivyomo katika mazingira	Kutaja vitu vilivyomo katika mazingira
	Kusafisha mazingira	Kufanya usafi wa mazingira
	Kuchukua tahadhari	Kutambua alama za tahadhari Kutaja mazingira hatarishi Kueleza namna ya kuchukua tahadhari
Kumudu Stadi za Kisanii	Kumudu sanaa za ubunifu zinazohusisha utendaji wa mikono	Kuchora picha, Kuumba/ kuunda vitu mbalimbali, Kupaka rangi, Kutia nakshi Kusuka
	Kumudu sanaa za ubunifu zinazohusisha utendaji wa mwili	Kuvuta pumzi Kufanya mijongeo mbalimbali Kucheza michezo mbalimbali Kulenga shabaha
	Kumudu sanaa za ubunifu wa sauti	Kuimba nyimbo Kutamba ngonjera Kughani mashairi Kuigiza sauti na milio Kusimulia hadithi
Kutumia Dhana za Kihisabati	Kuainisha vitu mbalimbali katika mazingira ya shule	Kutaja vitu katika mazingira Kuonesha rangi mbalimbali Kupanga vitu kulingana na sifa Kulinganisha na kutofautisha vitu
	Kubaini dhana ya wakati	Kutaja nyakati za siku Kufanya matendo kulingana na wakati Kutaja siku za juma
	Kumudu stadi za vipimo	Kulinganisha vitu vingi na vichache, virefu na vifupi, vinene na vyembamba, vikubwa na vidogo.
	Kujenga dhana ya namba	Kutamka majina ya namba 1-10 Kufanya matendo rahisi ya kuhesabu namba Kupanga vitu kwa idadi Kuhesabu namba 1-10

4.8 Uthibiti wa Ubora

Uthibiti wa ubora wa ujifunzaji na ufundishaji katika Elimu ya Awali utahusisha makundi mbalimbali kulingana na ngazi za kimamlaka. Ngazi hizo ni Shule, Kata, Wilaya, Mkoa na Taifa. Maofisa mbalimbali wa serikali ambao ni Mwalimu Mkuu, Ofisa Elimu Kata, Ofisa Elimu wa Wilaya, Ofisa Elimu wa Mkoa na Wathibiti Ubora katika Wilaya, Kanda na Taifa watashiriki kikamilifu katika kufuatilia na kuthibiti ubora wa ufundishaji na ujifunzaji wa Elimu ya Awali. Uthibiti wa ubora ufanyike kwa kuzingatia mwongozo wa uthibiti wa ubora ulioandaliwa na WESTU.

4.9 Ufuatiliaji na Tathmini

Ufuatiliaji wa utekelezaji wa mtaala unahusisha wadau mbalimbali wa ndani na nje ya shule. Lengo kuu la ufuatiliaji ni kuona iwapo utekelezaji unafanyika kama ilivyopangwa na kutoa mapendekezo ya kuboresha. Ni muhimu utaratibu mzima wa ufuatiliaji ulenge makuzi jumui ya mtoto. Wahusika katika ufuatiliaji wa utekelezaji wa mtaala ni Mwalimu Mkuu, Kamati za Shule, Wazazi, Ofisa Elimu Kata, Wamiliki wa Shule za Awali na Msingi zisizo za Serikali, Wathibiti Ubora wa Elimu ngazi ya Kata, Wilaya, Kanda na Taifa na Ofisa Elimu Wilaya na Mkoa. Wengine ni TET, Baraza la Mitihani, WESTU, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR-TAMISEMI) na asasi zisizo za kiserikali zinazojihusisha na elimu.

Tathmini ya ubora inahusu ukusanyaji wa taarifa za ufanisi na matokeo ya shughuli mbalimbali katika shule kwa kuzingatia malengo yaliyowekwa. Kupitia tathmini, shule itajifunza kuhusu nini kifanyike na hivyo kuweka mipango madhubuti itakayoboresha Elimu ya Awali. Majukumu ya wafuatiliaji na watathmini wa utekelezaji wa mtaala wa Elimu ya Awali yameainishwa kwa ujumla katika Kiunzi cha Kitaifa cha Elimu ya Awali.

4.10 Usimamizi wa Mtaala

Usimamizi wa utekelezaji wa mtaala wa Elimu ya Awali utafanywa katika ngazi mbalimbali kuanzia ngazi ya shule hadi wizara. Msimamizi katika ngazi ya shule ni Mwalimu Mkuu, ngazi ya kata ni Ofisa Elimu Kata, ngazi ya Wilaya ni Ofisa Elimu Wilaya, ngazi ya Mkoa ni Ofisa Elimu Mkoa na ngazi ya Wizara ni Mkurugenzi wa Kitengo cha Elimu ya Msingi.

4.11 Mafunzo Endelevu ya Mtaala kwa Walimu

Katika utekelezaji wa mtaala wa Elimu ya Awali, kutakuwa na mafunzo endelevu kwa walimu kuhusu utekelezaji wa mtaala. Mafunzo haya yatawasaidia walimu kuutekeleza mtaala kwa ufanisi zaidi ili kumwezesha mtoto kujenga umahiri uliokusudiwa. Mafunzo haya yatatolewa kupitia njia mbalimbali zikiwemo warsha/semina, masafa au kozi fupi kulingana na mahitaji yaliyopo. Vilevile, mafunzo haya yatatolewa kwa wadau wengine wa Elimu ya Awali kulingana na mahitaji yao.

4.12 Ushiriki wa Wazazi/Jamii

Malezi, makuzi na maendeleo ya awali ya mtoto ni suala shirikishi ambalo huanzia katika ngazi ya familia kwa kushirikiana na jamii inayomzunguka mtoto. Hivyo ushiriki wa wazazi na jamii ni jambo muhimu katika uchangamshi wa awali wa mtoto ili kumwandaa kujiunga na elimumsingi. Ni muhimu kwa shule ya awali kushirikisha wazazi, familia na jamii katika ujifunzaji wa mtoto na kuhakikisha mtoto anapata mahitaji yake muhimu. Shughuli ambazo wazazi/jamii wanaweza kushirikishwa ni pamoja na:

(i) Kushiriki katika uamuzi wa uanzishaji na uendeshaji wa shule ya awali katika eneo lao;
(ii) Kuchangia nguvukazi kwa ajili ya maendeleo ya shule;
(iii) Kushiriki katika ufuatiliaji wa maendeleo ya mtoto shuleni na nyumbani;
(iv) Kushiriki katika ufundishaji na ujifunzaji wa mtoto kupitia njia mbalimbali kama vile kuandaa au kutoa vifaa vya kufundishia na kujifunzia, masimulizi ya hadithi na uandaaji wa mazingira ya kufundishia na kujifunzia; na
(v) Kushiriki katika kufanya tathmini ya maendeleo ya mtoto.

4.13 Ubia Kati ya Sekta ya Umma na Wadau Wengine

Serikali inatambua mchango wa wadau mbalimbali katika utoaji wa Elimu ya Awali kama ilivyoainishwa katika Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014. Ubia unalenga kuongeza uwezo wa sekta ya elimu na mafunzo katika kutoa huduma mbalimbali katika Elimu ya Awali. Ubia katika utoaji wa elimu hii utahusisha Serikali na wadau wengine kama vile sekta binafsi, Asasi Zisizo za Serikali (AZISE), Taasisi za kidini, Wabia wa Maendeleo ya Elimu, Watafiti, Watu Binafsi na Vyombo vya habari.

SEHEMU YA PILI

MUHTASARI WA ELIMU YA AWALI

1.0 Utangulizi

Muhtasari ni kifaa cha mtaala ambacho kimebeba umahiri ambao mtoto anapaswa kuujenga. Mwalimu anapaswa kuandaa azimio la kazi na andalio la somo linalozingatia misingi ya ufundishaji wa elimu ya awali na kuhakikisha kuwa mtoto anajenga umahiri uliokusudiwa. Pia anasisitizwa kutumia viashiria pendekezwa vya utendaji vilivyoainishwa katika muhtasari huu ili kubaini kama mtoto amejenga umahiri huo. Hata hivyo, katika baadhi ya maeneo mwalimu anaweza kuandaa shughuli za ziada ili kuwawezesha watoto kumudu umahiri uliokusudiwa.

2. 0 Mpangilio wa Muhtasari

Jedwali la Muhtasari wa Elimu ya Awali limebeba maudhui ambayo yatafundishwa kwa mtoto wa Elimu ya Awali kwa muda wa mwaka mmoja. Maudhui haya yamepangiliwa katika vipengele vifuatavyo: Umahiri Mkuu, Umahiri Mahususi, Shughuli za Kutendwa na Mtoto, Viashiria Pendekezwa vya Utendaji na Idadi ya Vipindi. Mwalimu halazimiki kufuata mtiririko wa umahiri uliopo katika muhtasari wakati wa kufundisha, bali anapaswa kuhakikisha kwamba ufundishaji wa umahiri zenye mahusiano unakwenda sambamba. Yafuatayo ni maelezo mafupi kuhusu vipengele vya muhtasari.

2.1 Umahiri Mkuu

Umahiri mkuu ni uwezo wa kutenda jambo kwa usahihi na kwa ufanisi unaokusudiwa kufikiwa na mtoto baada ya kujifunza kwa muda fulani. Umahiri mkuu hujengwa na umahiri mahususi kadhaa hatua kwa hatua.

2.2 Umahiri Mahususi

Ni uwezo unaojengwa na mtoto katika kutenda shughuli mbalimbali kwa muda maalumu.

2.3 Shughuli za Kutendwa na Mtoto

Ni vitendo zinazofanywa na mtoto ili kujenga umahiri husika

2.4 Viashiria Pendekezwa vya Utendaji

Ni matendo yanayooneshwa na mtoto baada ya kujenga umahiri uliokusudiwa kwa kipindi fulani

2.5 Idadi ya Vipindi

Ni kadirio la muda utakaotumika katika ufundishaji na ujifunzaji kwa kuzingatia uzito wa umahiri mahususi na shughuli za kutenda mtoto. Kadirio hili la muda limewekwa kwa mfumo wa vipindi ambapo kila kipindi ni dakika 20. Hata hivyo, mapendekezo haya ya idadi ya vipindi yanaweza kubadilika kulingana na mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji.

3.0 Maudhui ya Muhtasari

UMAHIRI MKUU	UMAHIRI MAHUSUSI	SHUGHULI ZA KUTENDWA NA MTOTO	VIASHIRIA PENDEKEZWA VYA UTENDAJI	IDADI YA VIPINDI
Kuhusiana	Kujali	Kutambulishana	Kutaja jina lake kamili Kutaja mahali anapoishi Kutaja jina la shule Kutaja majina ya watu wengine yanayoonesha uhusiano.	20
		Kushirikiana katika kazi mbalimbali.	Kutatua tatizo Kupeana zamu katika kazi na michezo Kuchangia vitu/ kutumia vitu pamoja Kuvumiliana Kusaidiana.	
	Kuheshimiana	Kusalimiana kwa kuzingatia rika.	Kutoa na kuitikia salamu kwa usahihi.	30
		Kubainisha matendo ya Tabia njema.	Kutumia lugha inayokubalika Kuomba vitu Kushukuru Kuomba msamaha.	
		Kubainisha mavazi yanayokubalika kulingana na mazingira.	Kutaja mavazi yanayokubalika kulingana na mazingira.	
	Kujitawala	Kufanya vitendo vya kujitegemea.	Kuvaa mavazi yake mwenyewe Kufanya usafi wa mwili wake Kunawa mikono Kuchana nywele Kufanya kazi kula mwenyewe.	30

UMAHIRI MKUU	UMAHIRI MAHUSUSI	SHUGHULI ZA KUTENDWA NA MTOTO	VIASHIRIA PENDEKEZWA VYA UTENDAJI	IDADI YA VIPINDI
		Kutumia njia zinazokubalika kutawala hisia.	Kuonesha uvumlivu, furaha na upendo, Kufuata taratibu za ratiba yake ya siku, Kusema anapojisikia uhitaji wa kitu, Kumudu mazingira mapya.	
		Kufanya vitendo mbalimbali vya kutunza vitu.	Kutunza vitu vyake na vya wengine mahali sahihi Kupanga vitu vyake sehemu sahihi Kutumia vitu kwa uangalifu	
Kuwasiliana	Kusikiliza	Kubainisha vitu vinavyotoa sauti au milio.	Kutaja vitu vinavyotoa sauti au milio.	40
		Kusikiliza nyimbo, mazungumzo na hadithi fupi.	Kuelezea ujumbe unaotokana na nyimbo, mazungumzo na hadithi aliyosikiliza.	
		Kusikiliza maelekezo/maagizo	Kutenda kulingana na maelekezo, kanuni, maagizo, na taratibu zilizotolewa.	
		Kucheza mchezo wa kupashana habari.	Kusikiliza na kutoa ujumbe kwa usahihi.	
	Kuzungumza	Kujadiliana.	Kutumia lugha kwa usahihi. Kutamka maneno kwa usahihi. Kujadiliana kwa kuzingatia taratibu za majadiliano Kujieleza.	

UMAHIRI MKUU	UMAHIRI MAHUSUSI	SHUGHULI ZA KUTENDWA NA MTOTO	VIASHIRIA PENDEKEZWA VYA UTENDAJI	IDADI YA VIPINDI
		Kubaini vitendawili mbalimbali.	Kutega na kutegua vitendawili.	
		Kuimba nyimbo mbalimbali.	Kutamka maneno kwa usahihi. Kuimba nyimbo.	
		Kusimulia hadithi mbalimbali.	Kubaini maneno mapya Kueleza ujumbe uliokusudiwa katika hadithi.	
		Kuelezea shughuli za kila siku.	Kutaja shughuli za kila siku kulingana na wakati na mazingira Kutamka maneno kwa usahihi Kutumia maneno kwa usahihi.	
		Kueleza vitu anavyovipenda na asivyovipenda.	Kubainisha vitu anavyovipenda na asivyovipenda.	
	Kumudu stadi za awali za Kusoma.	Kusoma picha	Kuelezea picha alizozisoma Kuonesha hisia zake wakati wa kusoma picha.	
		Kujenga uelewa kuhusu vitabu/ machapisho.	Kubaini vitabu/ machapisho mbalimbali. Kufungua vitabu/ machapisho kutoka kushoto kwenda kulia Kubainisha kuwa maandishi huandikwa kutoka kushoto kwenda kulia.	
		Kubaini majina/ maneno mbalimbali katika mazingira yake.	Kutaja majina/ maneno mbalimbali kwa usahihi.	

UMAHIRI MKUU	UMAHIRI MAHUSUSI	SHUGHULI ZA KUTENDWA NA MTOTO	VIASHIRIA PENDKEZWA VYA UTENDAJI	IDADI YA VIPINDI
		Kubaini sauti za mwanzo za majina ya watu/vitu katika mazingira yake.	Kutamka sauti ya mwanzo ya majina ya watu,wanyama na vitu.	
		Kutaja majina ya vitu vyenye sauti za mwanzo zinazofanana.	Kutamka majina ya vitu vyenye sauti za mwanzo zinazofanana.	
		Kubainisha sauti za irabu na konsonanti.	Kutamka sauti za irabu na konsonanti kwa usahihi.	
	Kumudu stadi za awali za kuandika.	Kufanya mazoezi ya kuimarisha misuli ya mikono na vidole	Kumudu kushika vitu mbalimbali.	60
		Kufanya mazoezi ya kutumia vichoreo / viandikio	Kukaa mkao sahihi wakati wa kuandika Kushika vichoreo na viandikio kwa usahihi.	
		Kufanya mazoezi ya kuchora mistari kutoka kushoto kwenda kulia na kutoka juu kwenda chini.	Kuchora mistari kutoka kushoto kwenda kulia na kutoka juu kwenda chini.	
		Kuumba/kuunda maumbo ya irabu.	Kutengeneza vifani vya maumbo ya irabu.	
		Kufuatisha maumbo ya irabu.	Kufuatisha maumbo ya irabu.	
		Kuandika herufi za irabu kwa kufuata hatua .	Kuandika herufi za irabu hewani, kwenye mchanga, kibao na kwenye daftari.	

UMAHIRI MKUU	UMAHIRI MAHUSUSI	SHUGHULI ZA KUTENDWA NA MTOTO	VIASHIRIA PENDKEZWA VYA UTENDAJI	IDADI YA VIPINDI
		Kuumba/kuunda maumbo ya konsonanti	Kutengeneza vifani vya maumbo ya konsonanti	
		Kufuatisha maumbo ya konsonanti	Kufuatisha maumbo ya konsonanti	
		Kuandika herufi za konsonanti kwa kufuata hatua.	Kuandika herufi za konsonanti hewani, kwenye mchanga, kibao na kwenye daftari.	
Kutunza Afya	Kubainisha sehemu za nje za mwili na kazi zake.	Kutaja sehemu za nje ya mwili wake.	Kuonesha sehemu za nje za mwili wake.	30
		Kubaini kazi za sehemu za mwili.	Kuelezea kazi za sehemu ya mwili.	
		Kutumia milango ya fahamu kubaini vitu katika mazingira.	Kubaini vitu mbalimbali kwa kutumia milango ya fahamu.	
	Kutunza mwili.	Kubaini vifaa vya kufanyia usafi wa mwili.	Kutaja vifaa vya kufanyia usafi wa mwili.	40
		Kufanya usafi wa mwili.	Kumudu kupiga mswaki, kunawa uso, kuchana nywele, kunawa mikono kwa maji na sabuni kwa kufuata hatua.	
		Kueleza umuhimu wa kufanya usafi wa mwili.	Kutaja umuhimu wa kufanya usafi wa mwili.	

UMAHIRI MKUU	UMAHIRI MAHUSUSI	SHUGHULI ZA KUTENDWA NA MTOTO	VIASHIRIA PENDKEZWA VYA UTENDAJI	IDADI YA VIPINDI
		Kufanya mazoezi ya kukunja nguo ndogondogo.	Kueleza umuhimu wa kukunja nguo Kukunja nguo.	
		Kueleza umuhimu wa kufanya usafi wa nguo.	Kueleza umuhimu wa kufanya usafi wa nguo.	
		Kuvaa viatu.	Kuvaa viatu kwa usahihi. Kueleza umuhimu wa kuvaa viatu.	
	Kutunza vyombo vya chakula.	Kubaini vyombo vinavyotumika kulia chakula.	Kutaja vyombo vinavyotumika kulia chakula.	
		Kubaini vifaa vinavyotumika kufanya usafi wa vyombo vya chakula.	Kutaja vifaa vya kusafishia vyombo vya chakula.	
		Kufanya usafi wa vyombo vya chakula.	Kuosha vyombo vyake vya chakula. Kukausha vyombo vyake baada ya kuviosha.	
		Kubainisha sehemu za kuhifadhi vyombo vya chakula.	Kutaja sehemu za kuhifadhi vyombo vya chakula.	
	Kubainisha chakula bora.	Kubaini vyakula vinavyopatikana katika mazingira wanamoishi.	Kutaja vyakula vinavyopatikana katika mazingira anayoishi.	40
		Kubainisha chakula bora.	Kutaja chakula bora.	
		Kuandaa chakula bora.	Kushiriki kuandaa chakula bora Kueleza umuhimu wa kula chakula bora.	
		Kula kwa kufuata taratibu.	Kutaja taratibu za kufuata kabla na baada ya kula. Kuonesha tabia njema wakati wa kula.	

UMAHIRI MKUU	UMAHIRI MAHUSUSI	SHUGHULI ZA KUTENDWA NA MTOTO	VIASHIRIA PENDKEZWA VYA UTENDAJI	IDADI YA VIPINDI
Kutunza Mazingira	Kubainisha vitu vilivyomo katika mazingira.	Kuainisha vitu katika mazingira.	Kutaja majina ya vitu vilivyo hai katika mazingira Kutaja majina ya vitu visivyo hai katika mazingira.	30
	Kusafisha mazingira.	Kubaini vifaa vya kufanyia usafi wa mazingira.	Kutaja vifaa mbalimbali vya kufanyia usafi wa mazingira.	20
		Kufanya usafi wa mazingira.	Kuonesha vitendo vya kufanya usafi wa mazingira. Kutupa takataka mahali panapostahili. Kuweka vitu katika mpangilio Kueleza umuhimu wa kufanya usafi wa mazingira.	
		Kubainisha vitu vinavyochafua mazingira.	Kutaja vitu vinavyochafua mazingira.	
	Kuchukua tahadhari.	Kubainisha vitu na maeneo hatarishi katika mazingira.	Kutaja vitu na maeneo hatarishi katika mazingira yake.	40
		Kuondoa vitu hatarishi katika mazingira.	Kuondoa kwa tahadhari vitu hatarishi vilivyo katika mazingira yake.	
		Kubainisha alama za tahadhari.	Kutaja alama za tahadhari. Kuelezea alama za tahadhari.	
		Kutenda matendo yanayohusisha kuchukua tahadhari.	Kueleza namna ya kuchukua tahadhari.	
Kumudu Stadi za Kisanii	Kumudu sanaa za ubunifu zinazohusisha utendaji wa mikono.	Kubaini sanaa za utendaji wa mikono.	Kutaja sanaa za utendaji wa mikono.	90
		Kuumba maumbo ya vitu mbalimbali.	Kuumba maumbo mbalimbali. Kuelezea vitu alivyoumba.	

UMAHIRI MKUU	UMAHIRI MAHUSUSI	SHUGHULI ZA KUTENDWA NA MTOTO	VIASHIRIA PENDKEZWA VYA UTENDAJI	IDADI YA VIPINDI
		Kuchora picha na maumbo.	Kuchora picha. Kuelezea picha alizochora	90
		Kupaka rangi katika vitu.	Kupaka rangi.	
		Kuunda vitu mbalimbali.	Kuunda vitu mbalimbali. Kuelezea vitu alivyounda.	
		Kutunga vitu mbalimbali.	Kumudu kutunga vitu.	
		Kutia nakshi katika vitu.	Kumudu kutia nakshi.	
		Kusuka vitu mbalimbali.	Kumudu kusuka vitu mbalimbali.	
	Kumudu sanaa za ubunifu zinazohusisha utendaji wa mwili.	Kubainisha sanaa za utendaji wa mwili.	Kutaja sanaa za utendaji wa mwili.	60
		Kufanya mazoezi ya kuvuta pumzi.	Kuvuta pumzi.	
		Kufanya mazoezi ya mijongeo mbalimbali.	Kumudu mijongeo mbalimbali.	
		Kulenga shabaha.	Kumudu kulenga shabaha.	
		Kucheza michezo mbalimbali.	Kumudu kunyanyua vitu vyepesi. Kumudu kusukuma na kuvuta vitu. Kumudu usawazishaji wa mwili. Kumudu kucheza michezo mbalimbali.	
	Kumudu sanaa za ubunifu wa sauti.	Kuimba nyimbo mbalimbali.	Kuimba nyimbo.	50
		Kutamba ngonjera.	Kutamba ngongera.	
		Kughani mashairi.	Kughani mashairi.	
		Kuigiza sauti na milio.	Kuigizi sauti na milio.	

UMAHIRI MKUU	UMAHIRI MAHUSUSI	SHUGHULI ZA KUTENDWA NA MTOTO	VIASHIRIA PENDKEZWA VYA UTENDAJI	IDADI YA VIPINDI
		Kutoa vichekesho.	Kuchekesha.	
		Kusimulia hadithi.	Kusimulia hadithi.	
Kutumia Dhana za Kihisabati	Kuainisha vitu katika mazingira ya shule.	Kubainisha vitu katika mazingira.	Kutaja vitu katika mazingira.	20
		Kubainisha rangi za msingi.	Kutaja rangi mbalimbali. Kutaja rangi za msingi Kuonesha rangi nyekundu, bluu na njano. Kuchora picha na kupaka rangi.	
		Kubainisha maumbo bapa.	Kutaja maumbo bapa. Kuchora maumbo bapa. Kupaka rangi maumbo bapa.	
		Kupanga vitu kulingana na sifa.	Kubainisha vitu katika makundi kulingana na sifa.	
		Kucheza michezo ya kufananisha na kutofautisha vitu.	Kufananisha na kutofautisha vitu.	
	Kujenga dhana ya wakati.	Kubaini nyakati tofauti za siku.	Kutaja nyakati za siku.	20
		Kuigiza matendo yanayofanywa kulingana na nyakati.	Kuonesha vitendo mbalimbali vinavyofanywa kulingana na nyakati.	
		Kubainisha siku za juma.	Kutaja majina ya siku za juma.	
		Kutofautisha siku katika juma.	Kutaja siku za kwenda shule na siku za mapumziko.	
	Kumudu stadi za vipimo.	Kulinganisha vitu kutokana na sifa zake.	Kubainisha vitu vingi na vichache, virefu na vifupi, vinene na vyembamba, vikubwa na vidogo.	20
	Kujenga dhana ya namba.	Kubainisha vitu vinavyosaidia kujenga dhana ya namba.	Kutaja vitu mbalimbali katika mazingira vinavyosaidia kujenga dhana ya namba. Kufanya matendo mbalimbali kwa mpangilio yanayojenga dhana ya namba.	100
		Kutamka namba 1-10.	Kutamka namba kwa usahihi 1-10.	

UMAHIRI MKUU	UMAHIRI MAHUSUSI	SHUGHULI ZA KUTENDWA NA MTOTO	VIASHIRIA PENDKEZWA VYA UTENDAJI	IDADI YA VIPINDI
		Kufanya vitendo rahisi vya kuhesabu namba.	Kuhesabu namba kwa vitendo.	
		Kuhesabu namba kwa kutumia vitu.	Kutaja majina ya namba 1 -10.	
		Kulinganisha idadi ya vitu na namba.	Kulinganisha idadi ya vitu na namba.	
		Kufanya matendo ya kuongeza na kupunguza vitu.	Kuongeza na kupunguza vitu kwa usahihi.	
		Kubainisha maumbo ya namba kwa kutumia vitu mbalimbali.	Kufananisha maumbo ya namba na vitu mbalimbali.	
		Kuumba/kuunda maumbo ya namba.	Kuumba/kuunda maumbo ya namba.	
		Kufuatisha maumbo ya namba.	Kufuatisha maumbo ya namba kwa usahihi.	
		Kuandika namba kwa kufuata hatua.	Kuandika namba hewani, kwenye mchanga, kibao na kwenye daftari.	